

Learning by Ear Illiteracy**“A GIRL FINISHING SCHOOL”****Episode 03:** *“Barua ya Elinam”***Author:** Frédéric GAKPARA**Editor:** Yann Durand**Translator:** Anne Thomas

Characters: **Latifa** (*Ana umri wa miaka 15. Ni binti yao Papa Wali na Mamoua. Mwaka wa tisa huu anaosoma. Ni mwerevu kiasi kwamba hajawahi kurudia darasa lolote. Hata hivyo anakabiliwa na tatizo la wazazi wake kutaka kumwachisha masomo.*)

Zakia (*Ana umri wa miaka 20, ni msichana aliye na uhuru wa kujitendea mambo, ni rafiki yake Latifa na amejiriwa katika afisi ya wakala wa Utalii kutokana na tajriba yake ya kimasomo. Ni msichana aliyebahatika kutembelea mahali pengi na hukutana na watu wengi kazini mwake.*)

Papa Wali (*Baba wa watoto watatu, mwenye umri wa miaka 52 – Mtoto wake wa kwanza wa kiume anaitwa Elinam, kisha anafuatwa na binti aitwaye Latifa na mwisho mtoto wa kiume aitwaye Jaurès. Anashughulika na karakana ya vyuma lakini hajui kusoma na kuandika. Biashara inamwendea vibaya kila kukicha kwa kuwa hajamudu kujifunza mbinu mpya za ufundi hivi kwamba hamudu ushindani mpya wa kibiashara.*)

Epiphane (*Mvulana wa umri wa miaka 18, amejiriwa na Papa Wali. Ni mwerevu sana lakini hawezi kusoma wala kuandika kwa kuwa hakupata fursa ya kujiunga na shule. Kadiri anavyopata shida kutoka na hali yake hiyo ya kutojua*

kusoma, ndivyo hamu yake ya kujua kusoma na kuandika inavyozidi.)

Mamoua (*Mwenye umri wa 39 , mke na mama ya watoto wa Papa Wali. Ni mjamzito wa mtoto wao wa nne. Hajui kusoma na kuandika. Anafanya biashara ndogo ya kuuza uji wa unga wa mahindi mbele ya nyumba yao.*)

Teacher (*Mwanamume mwenye umri wa miaka 36, mwalimu katika shule ya kina Latifa, anampenda sana Latifa kwasababu ya werevu wake na matokeo yake mema shuleni*)

INTRO

*Hamjambo na karibu kwenye kipindi cha Noa Bongo Jenga Maisha Yako katika makala ya tatu ya mfululizo wetu wa “**Mtoto wa kike ahitimu**” kuhusu elimu na kutojua kusoma na kuandika. Latifa amekuwa nyumbani kwa kiasi cha wiki mbili kufikia sasa. Amekuwa akifanya kazi za nyumbani na kuuza uji tangu alipofukuzwa shule kwa sababu ya kutolipiwa karo. Baba yake anamtuma kwenda posta anakotumaini kuwa atapata barua kutoka kwa kaka yake Elinam. Kweli anaipata barua. Ingawa anatamani sana kuifungua hiyo barua kujua kilichomo, anakwenda kazini kwa rafiki yake Zakia kabla ya kumpelekea baba yake barua. Sikiliza yatakavyokuwa katika sehemu ya tatu ya” **Barua ya Elinam**”.*

Scene 1, IN ZAKIA'S OFFICE

Zakia na Latifa

1. SFX ATMO: OFFICE SOUNDS. SOUND OF STEPS AND KNOCKING

2. Zakia: Naam, Karibu ndani!

3. SFX: THE DOOR OPENS AND CLOSES

4. Zakia: Alaa Latifa! Sikujua ulikuwa njiani! Cha mno? Hujambo?

5. Latifa: (Excited) Sijambo Zakia! Baba ndiye amenituma... amenituma posta... Na wajua nilichopata?!!!

6. Zakia: (Spontaneously) Barua ya Elinam!

7. Latifa: Ndiyo, lakini hatuwezi kuifungua.

8. Zakia: Lakini tunaweza kukisia ujumbe wake.... mm, ebu tukisie... (**Changes voice**) *Kwa Baba, kama nilivyokwambia tulipowasiliana kwa simu, ingekuwa bora mdogo wangu Latifa asikatiziwe masomo yake. Nani ajuae? Pengine huenda akawa muokozi wa familia nzima! Nadhani anaweza hata kuwa mwanasiasa siku za usoni!*

9. Latifa: (Laughter) Kweli? Mwanasiasa aliyemakinika! (**becoming serious again**) Zakia, ninachelea mambo yawe vingine. Pengine hatma yangu imo ndani ya barua hii. Hebu fikiria!

10. Zakia: Naam. Wajua?

11. SFX: TELEPHONE RINGS

12. Zakia: Nipe muda kidogo, Latifa... (**Picks up**) Hallo! (...) Hallo, Sir! (...)
Ndiyo, Wamewasili hivi punde. (...) Kiasi dakika kumi na tano, Sir! (...)
Naam, Tutakwenda kwenye jumba la makumbusho. Baada ya chakula cha
mchana, tutakwenda kwenye soko la kitamaduni kununua zawadi. (...) Naam,
Naam! Leo ni siku ya kununua vitu! Kesho tutatembelea maeneo ya
kumbukumbu za kihistoria. (...) Naam! (...) Asante.

13. SFX: TELEPHONE BEING HUNG UP

14. Zakia: Huyo mkuu wangu kazini, yaani mkurugenzi mtendaji. Ninapaswa
kuandamana na watalii. Sitakuweco ofisini mchana kutwa na pengine juma
zima lijalo.

15. Latifa: Bila shaka unaifurahia kazi yako. Natamani ningeandamana na
wewe.

16. Zakia: Kwa bahati mbaya haiwezekani kwani hairuhusiwi kusafiri kwa basi
la watalii bila kukatiwa bima. Tuzungumzie hii barua... ngoja tupange.

17. Latifa: Enhe....

18. Zakia: Kwa vile wewe ndiye unayemsomea barua zake, kwanza jisomee
kwa makini barua yenyewe.

19. Latifa: Naam, nitafanya hivyo....

20. Zakia: Twaa fedha hizi , kama tulivyopanga, kisha utamwambia babako
kwamba umezipata posta na kwamba Elinam ndiye aliyekuletea.

21. Latifa: Naam, Sawa.

22. Zakia: Uhakikishe kwamba barua hiyo ujumbe wake hauendi kinyume na kisa chako hicho. Ingawa siamini kwamba Elinam atabadilisha mawazo na kuandika mambo tofauti.

23. Latifa: (Evasive) Natumai ni hivyo...

24. Zakia: Changamka nawe! Usifikirie mabaya tu!

25. SFX: **OPENING DRAWER + NOTES BEING COUNTED**

26. Zakia: Fedha hizi. Utaweza kulipa karo yako na ada ya mtihani.

27. Latifa: Zakia...

28. Zakia: Enhe? Inanibidi niondoke upesi. Watalii wangu wananisubiri!

29. SFX: **COMPUTER BEING TURNED OFF**

30. Latifa: Asante sana! Asante sana! Mungu naye atakulipa kwa wema wako huu!

31. Zakia: Tuyaachie Mungu hayo! Twen'zetu!

32. SFX ATMO: CHAIR + ARMCHAIR + DOOR BEING OPENED AND CLOSED + KEYS + SOFT BACKGROUND NOISE OF TOURISTS IN THE CORRIDOR

33. Zakia: (Kisses Latifa good bye) Kila la heri.

34. Latifa: Asante, Zak... Ninakutakia safari njema!

35. Zakia: Asante! Kwaheri! (Talking to the tourists in the corridor)
Mabibi na mabwana mnaombwa nyote muingie kwenye basi,
tutaondoka hivi punde.

36. SFX ATMO: SOUND OF STEPS AND VOICES

MUSIC

NARRATOR: *Papa Wali anasinzia kwenye karakana yake. Mfanyikazi wake, Epiphane anafua chuma huku akiimba. Latifa amewasili akiwa na hamu kubwa ya kuifungua barua aisomee mwenyewe badala ya kumsomea baba yake.*

Scene 2, IN PAPA WALI'S WORKSHOP

Papa Wali, Latifa na Epiphane

37. Epiphane: (Humming)

38. SFX ATMO: METAL SAW + HAMMER

39. Epiphane: Karibu, Latifa!

40. Latifa: Asante sana! Epiphane hujambo!

41. Epiphane: U hali gani?

42. Latifa: Sijambo! Babu yupo?

43. Epiphane: Naam, Yuko ndani.

44. Latifa: Asante! (**She starts off**)

45. Epiphane: Alaa, Mbona haraka hivyo?

46. Latifa: (**From afar**) Naam, nina haraka.

47. SFX ATMO: METAL SAW + HAMMER

48. Papa Wali: (**Snoring**)

49. Latifa: Shikamoo, baba! (**No answer**) Baba!

50. Papa Wali: (**He wakes up with a start**) Nini? Nini?

51. Latifa: Samahani! Shikamoo!

52. Papa Wali: (**Sounding sleepy**) Naam... Marahaba... Nini cha mno?

53. Latifa: Ulinituma posta. Kulikuwa na barua yako kutoka kwa Elinam na ndiyo sababu nimepitia hapa nikukabidhi.

54. Papa Wali: (**Yawning loudly and stretching out**) Nipe hiyo barua!

55. SFX: ENVELOPE BEING OPENED + LETTER BEING UNFOLDED

56. Papa Wali: (He gives her the letter) Isome! Ketu kwa pale.

57. SFX: CHAIR BEING PULLED OUT

58. Latifa: (Reading the letter) *Mpendwa baba. Natumai wewe, mama, Latifa na Jaurès mu wazima. Baba usinihangahikie sana. Hapa nilipo ninawasomesha baadhi ya wanafunzi na ninaweza kujilipia kodi ya nyumba. Kwa hivyo ningependa Latifa (Reading more slowly) arejee shuleni. (Silence).*

59. Papa Wali: Ni hayo tu?

60. Latifa: Bado naendelea Baba. (Carrying on) *Najua kwamba sasa hivi mna matatizo ya kifedha. Ndiposa nimewatumia fedha hizi kugharamia karo yake yote ya mwaka huu...*

61. SFX: ENVELOPE BEING CREASED

62. Papa Wali: (Looking in the ripped envelope) Fedha zi wapi?

63. Latifa: Hizi hapa.

64. Papa Wali: (Taking it) Mbona umezichukuwa wewe?

65. Latifa: Nimepewa hizo fedha posta kando na barua.

66. Papa Wali: Ni ngapi?

67. Latifa: Yuro sitini.

68. Papa Wali: Una hakika kwamba hicho ndicho kiasi cha fedha alicholeta?
(He counts)

69. SFX: COUNTING BANKNOTES

70. Latifa: Unaweza kumpigia simu Elinam alithibitisha hilo, Baba!

71. Papa Wali: Endelea kusoma barua. (He carries on counting and recounting.)

72. Latifa: (Starts reading again and insists on each word) *Ndiposa nawaletea hizi fedha kugharamia karo yake yote ya mwaka huu. Kumbuka fedha zote ambazo tayari umetumia kumsomesha. Mpe fursa ya kuendelea na masomo. Inambidi kufanya mtihani wake na tunahitajika sote kumuunga mkono. Pengine atahitaji kufanya kazi ya ziada kwasababu ya kukosa shule kwa muda. Mpeni nafasi ajiandae na ingekuwa bora mukimuomndolea majukumu ya kupika uji kila alfajiri.*

73. Papa Wali: (**Finally stopping his counting**) *Na mumuondolee majukumu ya kupika uji kila alfajiri?* Elinam anathubutu kuniambia hivyo! (**Raising his voice**) Mwambie huo uji ndio unaotulisha sasa hivi. Anaandika mambo kama hayo kwasababu ya Yuro sitini! Amejiunga na chuokikuu juzi juzi.

Tumeshawaharibu watoto nyie. Zichukue hizi hapa! Ni zako. Usije ukasema kwamba ninatumia fedha zako kulipia madeni yangu. Una hiari ya kuondoka!

74. Latifa: Lakini Baba, sijamaliza kusoma barua.

75. Papa Wali: Una lazima niyasikilize haya! Mmekuwa mkipanga njama nyie. Haye, endelea, Ninasikiliza!

76. Latifa: *Baba, ninatumai kwamba utamshawishi mama kuuona umuhimu wa hatua hii kwa manufaa yetu sote. Asante sana kwa mema uliyotutendea mpaka sasa. Mapenzi yako, malezi yako kwetu sisi na ucheshi wako. Kila la heri. Tutakutana hivi karibuni. Salamu kwa wote, Elinam.*

77. Papa Wali: Imeisha?

78. Latifa: Naam, Baba!

79. Papa Wali: Kwa hivyo hakuna fedha nilizoletewa mimi. Isipokuwa hiyo asante, asante. Amesema yote kuhusu “*mapenzi*” na mengineyo, faida yake ni “*asante*” (**He sighs**) Watoto wa Papa Wali!! (**Shouting**) Ninajitahidi iwezekanavyo ili nipate kukulipia kodi yako ya nyumba na ukibahatika kupata fedha kidogo huna jengine la kukumbuka ila elimu ya mdogo wako wa kike? Wala hakuna (**changes his voice**) “*Baba twaa Yuro hii moja ujinunulie chupa moja ya bia*” Oh! (**In a soft voice to Latifa**) Latifa!

80. Latifa: Beeh?

81. Papa Wali: Kabla ya kwenda nyumbani, nenda moja kwa moja hadi shuleni ukalipe karo. Utarejea shuleni kesho.

82. Latifa: Asante, Baba!

83. Papa Wali: (**Grumbling**) Mambo ni yayo hayo, Asante Baba! Hizo asante huliwa? (**Very firmly**) Zitwae fedha zitakazobaki! Siwezi tena kugharamia nakala za vitabu.

84. Latifa: Naam, Baba.

85. Papa Wali: Nitashauriana na mamako leo usiku. Tuombe Mungu kwamba atazingatia tutakayozungumza!

86. SFX: **STEPS GOING AWAY**

87. Papa Wali: (**Alone**) Haya, Wali! Hapo umepunguziwa tatizo moja...

88. SFX ATMO: WELDING MACHINE

MUSIC

NARRATOR: *Wakati Latifa, aliye na furaha si haba, anapokwenda kulipa karo, mwalimu wake anamtembelea mama yake, Mamoua. Yuko nje ya nyumba kwenye banda lake la uji na anaonekana kuwa mchovu.*

Scene 3, AT PAPA WALI'S HOME

Mamoua na mwalimu

89. SFX ATMO: HENS INSIDE + LITTLE TRAFFIC + PASSERSBY AND CHILDREN PLAYING

90. Teacher: Mama, hujambo!

91. Mamoua: (Exhausted) Sijambo! (Yawning) Unataka kiasi gani?

92. Teacher: Sitaki chochote, asante shangazi. Naitafuta nyumba ya kina Latifa.

93. Mamoua: Umefika.

94. Teacher: Yupu?

95. Mamoua: Hayupo. Kuna nini?

96. Professor: Mimi ni mwalimu wake. Hajaja shuleni kiasi cha majuma mawili hivi yaliyopita. Nimekuja kumjulia hali.

97. Mamoua: Alaa! Kumbe wewe ni mwalimu wake! Alifukuzwa shuleni kwa kuwa karo yake haikuwa imelipwa.

98. Teacher: Je wewe ndiye mamake?

99. Mamoua: Ndiye mimi!

100. Teacher: Lakini wengine waliofukuzwa wamesharudi. Kwani hukwenda kumshughulikia?

101. Mamoua: (**Very embarrassed and hesitant**) Eeeh... Babake hataki Latifa aendelee na masomo.

102. Teacher: Kwanini?

103. Mamoua: Babake aliamua hivyo.

104. Teacher: Lakini Latifa ni mwanafunzi mzuri sana. Si vizuri kumlazimisha kukatiza masomo yake. Huo si uamuzi mzuri, mama.

105. Mamoua: Si uamuzi wangu.

106. Teacher: Basi vyema kuzungumza na baba yake. Huenda mkamharibia binti yenu maisha yake ya usoni. Nitashauriana na mwalimu mkuu. Mama ninaondoka sasa. Mwambie Latifa kwamba mwalimu wake wa hesabu alikuja kumtazama.

107. Mamoua: Nitamwambia. Kwaheri mwalimu.

108. Teacher: Kwaheri, mama.

Music

OUTRO:

Mambo kangaja huenda yakaja. Mambo huenda yakamnyookea Latifa. Atarudi shuleni. Jee ataweza kujisimamia mwenyewe wakati wazazi wake wanapojitahidi kukabiliana na matatizo ya kifedha waliyo nayo? Ili kufahamu zaidi, sikiliza sehemu itakayofuata ya “Mtoto wa kike ahitimu”, mfululizo wa makala inayohusu elimu na kutojua kusoma na kuandika.

Ukitaka kukisikiliza tena kipindi hiki au vyengine vya mfululizo wa Noa Bongo Jenga Maisha Yako vya Deutsche Welle, tazama ukurasa wetu wa tovuti www.dw-world.de/lbe. Unaweza pia kutuandikia barua-pepe. Anwani ni: lbe@dw-world.de

Ahsante kwa kutusikiliza. Hadi wakati mwengine, Kwaheri!

END OF 3rd EPISODE